

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SERIKALI YA UJERUMANI YAMUAHIDI MAMBO MAKUBWA RC MAKONDA

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. PAUL MAKONDA leo ametembelewa Ofisini kwake na Balozi wa Ujerumani Nchini Tanzania DETLEF WAECHTER na kufanya nae Mazungunzo.

Katika Mazungunzo hayo yalijikita kwenye Mikakati ya pamoja kwenye Maboresho ya Sekta za Afya, Elimu, Usalama na Mapambano dhidi ya Dawa za kulevyva.

Kuhusu Sekta ya Elimu Balozi huyo ameguswa na kampeni ya Ujenzi wa Ofisi 402 za Walimu kwenye Mkoa wa Dar es Salaam ambapo ameahidi kushirikiana na RC MAKONDA katika kampeni hiyo.

Aidha RC MAKONDA amewasilisha kwa Balozi huyo ombi la kujengwa kwa Jengo la huduma ya Dharura (ICU) kwenye Hospital za Mkoa wa Dar es salaam ambapo Balozi amelichukuwa ombi hilo kwa ajili ya kulifanyia kazi.

RC MAKONDA amesema kuwa wamekubaliana kushirikiana katika mapambano ya Biashara ya Dawa za kulevyva pamoja na kutoa mafunzo ya namna ya kulinda Jiji kwa kutumia Teknolojia.

Balozi wa Ujerumani Nchini Bwana DETLET WAECHTER amesema watashirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika masuala yote ya Maendeleo.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

24/11/2017